



# Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | August-2026

EAJK


# Upembuzi wa Vigezo vya Upimaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya Sita Nchini Kenya


**Authors**

**Joyce Nechesa Burudi [(1)]; Fred Wanjala Simiyu [(2)]; Isaac Odeo Ipara [(3)]**

**Main author's email: jburudi70@gmail.com**

**(1.2.3) Kibabii University, Kenya.**



**Cite this article in APA**

Burudi, J. N., Wanjala, F. S., & Ipara, I. O. (2026). Upembuzi wa vigezo vya upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya Sita nchini Kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili,* 5(1), 113–124. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.1127

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026-06-17
Accepted: 2026-07-21
Published: 2026-08-19


Scan this QR to read the paper online


**Copyright:** ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).



**Ikisiri**

Utafiti huu ulitathmini mikakati ya upimaji wa stadi ya kuzungumza katika Gredi ya Sita (G6) magharibi mwa Kenya, uliolenga vigezo vya KICD na kuongozwa na Nadharia ya Mawasiliano ya Dell Hymes. Stadi ya kuzungumza ni kipaumbele katika Mtaala wa Umilisi (MU) nchini Kenya kwa ajili ya kukuza mawasiliano na ushirikiano. Utafiti ulitumia mkabala mseto na muundo wa usorovea fafanuzi katika kaunti nne za Kenya. Data ilikusanywa kutoka kwa walimu kupitia hojaji, mahojiano, na uchanganuzi wa nyaraka, kisha ikachanganuliwa kiwingiidadi na kithamano. Kati ya walimu 355 walioteuliwa kwa usampulishaji makusudi, walimu 341 (96%) walijaza hojaji kikamilifu. Matokeo makuu ya utafiti yanaonyesha kuwa ingawa walimu wengi wana uelewa wa mwongozo wa KICD unaozingatia vigezo sita vya tathmini ya kimilisi na kusisitiza matamshi pamoja na mijadala ya makundi, bado kuna udhaifu katika ufikiaji wa mwongozo huo na utekelezaji thabiti wa vipengele vya sarufi, msamiati, na ujasiri wa wanafunzi darasani. Kwa hitimisho, vigezo vya KICD vimefanikiwa kuimarisha uwezo wa kujieleza na matamshi ya wanafunzi wa Gredi ya Sita, lakini bado kuna haja ya kuziba mapengo yaliyopo. Ili kufikia ubora unaotarajiwa, utafiti unapendekeza kuwa taasisi za elimu ziharakishe usambazaji wa nyaraka za mtaala, zipanue maudhui ya warsha mbalimbali za walimu ili yajumuishe sarufi na msamiati, na ziingize kikamilifu matumizi ya teknolojia ya kisasa katika mchakato mzima wa upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili.



**Maneno muhimu:** Gredi ya sita, Kiswahili, mtaala wa umilisi, stadi ya kuzungumza, vigezo vya upimaji lugha.

## UTANGULIZI

Upimaji wa lugha ni kipengele cha msingi katika ufundishaji na huchukuliwa kama kilele cha mchakato wa kujifunza. Katika kiwango cha kimataifa, kuibuka kwa Mtaala unaozingatia Umilisi (MU) na stadi za Karne ya 21 kumeleta mabadiliko makubwa katika mbinu za upimaji, ambapo lengo limehama kutoka kukariri maarifa pekee hadi kupima uwezo wa mwanafunzi kutumia maarifa, stadi na mitazamo katika maisha ya kila siku (Care et al., 2018). Katika utekelezaji huu wa kimataifa, stadi za mawasiliano na lugha zimepewa kipao mbele kama nguzo kuu ya ujifunzaji wa kimilisi, ingawa upimaji wa stadi za kuzungumza na kusikiliza umekuwa ukikabiliwa na changamoto za kiufundi na za kitathmini kote ulimwenguni (Humphry et al., 2017).

Tafiti mbalimbali za kimataifa katika kiwango cha elimu ya msingi zimebainisha kuwa matumizi ya vigezo na zana maalum za tathmini ni nguzo muhimu katika kupunguza udhanifu na kuongeza utegemewa na uaminifu wakati wa kupima stadi ya kuzungumza lugha (Ahmad et al., 2021). Kwa mfano, tafiti zinazochunguza ufundishaji na upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni au ya pili katika nchi za kimataifa kama vile Marekani, Uingereza, Ujerumani, na Japan zimebainisha kuwa upimaji wa stadi za mdomo unakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa miongozo thabiti na vigezo vilivyosanifiwa vya utuzaji alama (Ahmad et al., 2021). Tafiti zilizofanywa katika vyuo na taasisi za elimu nchini Marekani na Ujerumani zimeonyesha kuwa waandaaji wa mitaala na walimu mara nyingi hujikita zaidi katika kupima stadi za kuandika na kusoma badala ya kutoa tathmini ya moja kwa moja ya stadi ya kuzungumza, kutokana na ugumu wa kiufundi wa kuandaa zana na vigezo sahihi vya upimaji wa mdomo (Djordjevic, 2024). Ukosefu huu wa vigezo vilivyowekwa wazi vya kupima utendaji wa mdomo husababisha walimu kutegemea uzoefu binafsi, jambo linalodhoofisha utegemewa wa matokeo ya upimaji wa wanafunzi.

Katika bara la Afrika, mataifa kadhaa ikiwemo Senegal, Cameroon, Rwanda na Tanzania yamekumbatia Mtaala wa Umilisi ili kulinganisha mifumo yao ya elimu na mahitaji ya kisasa ya soko la ajira na maendeleo ya kijamii (Lukindo, 2016). Hata hivyo, utekelezaji wa upimaji wa kimilisi barani Afrika umeendelea kukabiliwa na vikwazo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na maandalizi duni ya walimu, uhaba wa rasilimali za kufundishia na kutathminia, pamoja na msongamano wa wanafunzi madarasani, hali inayodhoofisha ufanisi wa upimaji endelezi na wa kiutendaji.

Nchini Kenya, utekelezaji wa Mtaala wa Mfumo wa Umilisi (CBC) tangu mwaka 2019 umebadilisha mtazamo wa upimaji kutoka mitihani ya jumla na ya kikomo hadi upimaji wa umilisi wa mwanafunzi. Kwa mujibu wa Taasisi ya Ukuaji wa Mtaala nchini Kenya (KICD, 2017), mtaala huu unasisitiza ukuaji wa stadi kuu nne za lugha: kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Mfumo wa tathmini nchini unajumuisha upimaji endelezi unaochangia asilimia 60 ya alama za jumla katika kiwango cha shule ya msingi na utathmini wa tamati unaosimamiwa na Baraza la Kitaifa la Mitihani la Kenya (KNEC). Upimaji huu endelezi huzingatia viwango au vigezo vinne vya utendaji: kuzidisha matarajio, kufikia matarajio, kukaribia matarajio na chini ya matarajio (KICD, 2021).

Pamoja na umuhimu wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili katika kukuza mawasiliano na uelewa wa kijamii na kitaaluma, upimaji wake darasani unakabiliwa na changamoto kubwa. Tafiti za awali nchini Kenya zinabainisha kuwa walimu hukumbwa na ugumu wa kuandaa kazi stahilifu na zana sahihi za kupima stadi hii, hali inayofanya matokeo ya upimaji kukosa utegemewa (Otieno & Machani, 2022). Zaidi ya hayo, ingawa Mtihani wa Tathmini ya Shule ya Msingi (KPSEA) unatumika kama tathmini ya tamati ya Gredi ya sita, haujumuishi kabisa kipengele cha upimaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili. Mtazamo huu wa KPSEA umeacha ombwe kubwa na tegemeo lote la tathmini ya stadi hii kuachiwa upimaji endelezi unaofanywa na walimu madarasani.

Hali hii inazua pengo kuu la maarifa, kwani ingawa tafiti zilizopo zimeangazia kwa ujumla changamoto za utekelezaji wa CBC nchini Kenya, hazijachunguza kwa kina ufaafu na ubora wa vigezo maalum vya upimaji vinavyotumiwa na walimu kupima Stadi ya Kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya sita. Kuna ukosefu wa utafiti unaobainisha iwapo vigezo vya ndani ya darasa vinawiana na misingi ya kiutathmini iliyowekwa na KICD na KNEC, au iwapo walimu wanamiliki uwezo wa kiufundi wa kuvitumia vigezo hivyo bila kuingiza udhanifu binafsi, hasa kwa kuzingatia kuwa mtihani wa kitaifa wa KPSEA haupimi

stadi hii. Pengo la maarifa pia linahatarisha uaminifu na utegemewa wa matokeo ya upimaji endelezi wa stadi ya kuzungumza katika kiwango hiki muhimu cha elimu ya msingi. Ili kuziba pengo hili, utafiti huu ulipembua vigezo vya upimaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya sita nchini Kenya.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Dhana ya Upimaji katika Mtaala wa Umilisi

Upimaji katika Mtaala unaozingatia Umilisi (MU) huchukua nafasi ya msingi kwa kuwa unaonyesha kile mwanafunzi anachojua, alichojifunza na anachohitaji kuboresha. Kwa mujibu wa Opondo et al. (2023), aina kuu za upimaji ni pamoja na upimaji wa wenza, upimaji endelezi na utathmini wa tamati, huku mfumo wa elimu nchini Kenya ukisisitiza zaidi upimaji endelezi. Upimaji huu hufanywa na walimu na hutoa mrejesho wa haraka unaomwezesha mwanafunzi kurekebisha mapungufu yake na kuimarisha matokeo ya ujifunzaji. Mfumo huu wa tathmini endelezi unagawanyika katika mwelekeo wa upimaji ili kujifunza na upimaji kama ujifunzaji. Upimaji ili kujifunza husaidia mwalimu kukusanya taarifa kuhusu utendaji wa mwanafunzi ili kuboresha mbinu za ufundishaji, wakati upimaji kama ujifunzaji humwezesha mwanafunzi kujipima, kutafakari na kuweka malengo ya kibinafsi; jambo ambalo ni muhimu katika kukuza ujasiri na kujisimamia wakati wa kuzungumza.

Katika kipengele hiki, tafiti zilizopo zinakubaliana kikamilifu kuwa upimaji wa stadi za lugha katika mtaala wa umilisi unapaswa kuwa endelevu badala ya kutegemea tathmini ya tamati pekee. Hata hivyo, udhaifu wa maandiko haya unajitokeza katika ngazi ya kiutendaji; watafiti hawa wanasisitiza dhana za kijumla za upimaji bila kufafanua jinsi walimu wanavyoweza kubadilisha dhana hizo kuwa zana halisi za kupima stadi ya kuzungumza darasani.

### Stadi ya Kuzungumza na Taratibu za Upimaji Wake

Stadi za lugha zimegawanyika katika makundi makuu mawili: stadi pokezi (kusikiliza na kusoma) na stadi zalishi (kuzungumza na kuandika) (Skolverket, 2019). Katika nadharia ya upatikanaji wa lugha ya pili, Krashen (1982) anabainisha kuwa stadi pokezi hutangulia zile zalishi. Mfumo huu unashikiliwa na Lightbown na Spada (2013), wanaobainisha kuwa kuzungumza ni stadi ngumu zaidi inayohitaji mazoezi ya kina ya kimaelezo na ujuzi wa matamshi, na hivyo upimaji wake unahitaji mbinu maalum zinazotofautiana na upimaji wa kusoma au kuandika. Kitaalamu, Eliyasun et al. (2018) wanafafanua kuzungumza kama njia ya kupitisha ujumbe kwa mdomo, huku Luoma (2004) akisisitiza umuhimu wake kama uti wa mgongo katika ufundishaji wa lugha. Zuhriyah (2017) anaongeza kuwa ukosefu wa ustadi wa kuzungumza huathiri ujasiri na uwezo wa mwanafunzi kuwasiliana ana kwa ana, jambo linalofanya upimaji wake uhitaji kuzingatia matumizi halisi ya lugha katika jamii.

Watafiti hawa wote wanakubaliana kuwa stadi ya kuzungumza ni yenye changamoto na inahitaji mbinu za kipekee za tathmini. Hata hivyo, kunajitokeza tofauti kubwa ya kimtazamo kati ya watafiti wa kileksika wanaosisitiza usahihi wa umbo la lugha (kwa mfano, matamshi na sarufi) na wale wa kimuktadha wanaosisitiza ufasaha na ujasiri wa mawasiliano. Pamoja na mchango wa tafiti hizi katika kubainisha sifa za stadi ya kuzungumza, mapungufu yao makuu yanatokana na kutoa mapendekezo ya kimfumo yanayoelea bila kuunda vigezo vya kupima utendaji vinavyoweza kutumiwa na walimu wa shule za msingi.

### Vigezo vya Upimaji wa Stadi ya Kuzungumza na Nyenzo za Tathmini

Vigezo vya upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili vinatofautiana kulingana na lengo na kiwango cha mawasiliano. Katika muundo wa mtaala wa Kenya, KICD (2021) inabainisha vigezo vya jumla kama vile matamshi, maamkuzi, heshima, matumizi ya methali na nahau, pamoja na ushirikiano. Katika uchambuzi wa meta unaoangazia vigezo vya msingi vya upimaji wa mdomo, Bimpong (2020) anataja uwezo wa kutamka maneno kwa usahihi, matumizi ya sarufi sahihi, ufasaha wa kuwasilisha hoja, na uwezo wa kushawishi hadhira. Mtazamo huu unapata usaidizi kutoka kwa Kretzer na Oluoch-Suleh (2022) wanaobainisha kuwa umilisi katika stadi za lugha unahusu pia ujenzi wa muktadha na uzalishaji wa mawazo katika mijadala na mazungumzo ya kila siku. Zaidi ya hayo, utafiti wa Osore (2022) uliopo katika ngazi ya shule za upili ulionyesha kuwa matumizi ya nyenzo za kusikiliza-kuona yanaboresha matamshi ya Kiswahili na yanafaa kujumuishwa katika zana za tathmini.

Aidha, utafiti wa Otieno na Machani (2022) ulilenga kuchunguza mbinu za tathmini darasani na changamoto zinazowakabili walimu katika utekelezaji

wa Mtaala wa Umilisi (CBC) katika shule za msingi nchini Kenya, ambapo matokeo yake yalibainisha kuwa ingawa walimu wana mtazamo chanya na uelewa wa misingi ya CBC, wengi wao hukabiliwa na ugumu katika maandalizi ya zana thabiti za utuzaji alama, uhaba wa nyenzo za kujifunzia, na idadi kubwa ya wanafunzi madarasani inayodhoofisha ufanisi wa upimaji endelezi. Kama walivyoeleza watafiti hao, "kuchanganua na kurekodi maendeleo ya mwanafunzi mmoja mmoja katika darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi kunahitaji muda na rasilimali ambazo mara nyingi hazipatikani kwa walimu wengi" (Otieno & Machani, 2022, uk. 18). Mfumo huu unaacha pengo la utafiti kwa sababu Otieno na Machani walizingatia tathmini ya jumla ya Mtaala wa Umilisi bila kuchanganua kwa undani viashiria mahsusi vya upimaji wa stadi mahsusi za lugha kama vile stadi ya kuzungumza Kiswahili katika gredi za juu za shule za msingi.

Kwa upande mwingine, utafiti wa Nyamai na Wambua (2023) ulichunguza matumizi ya mbinu shirikishi katika upimaji wa stadi za mawasiliano katika Kiswahili chini ya mtaala wa CBC, na matokeo yake yalionyesha kuwa matumizi ya mijadala ya vikundi, michezo ya kuigiza, na usimulizi wa hadithi huongeza uwezo wa wanafunzi katika ufasaha na matamshi sahihi ya Kiswahili sanifu. Watafiti hawa walisisitiza kuwa "upimaji wa stadi za lugha unapaswa kuvuka mipaka ya mitihani ya maandishi na kujikita katika kazi za vitendo zinazomwezesha mwanafunzi kuonyesha umilisi wa kiutendaji katika mazingira halisi ya kijamii" (Nyamai & Wambua, 2023, uk. 45). Hata hivyo, utafiti huu unaacha pengo la utafiti kwani uliangazia tu mbinu za ufundishaji na mwingiliano darasani bila kutathmini kiwango halisi cha walimu cha kufuata rubriki za KICD au kuchunguza athari za ukosefu wa mafunzo ya warsha kwa walimu wanaopima stadi hizo.

Uchambuzi wa makala haya ya awali unaonyesha makubaliano kuwa vigezo vya upimaji vinapaswa kupima pande mbili: usahihi wa kilugha na uwezo wa kimawasiliano. Hata hivyo, tofauti inajitokeza pale ambapo KICD (2021) inaelekeza vigezo vya kiutamaduni na kimaadili (kwa mfano, maamkuzi na heshima), ilhali watafiti wa kimataifa kama Bimpong (2020) wanajikita zaidi katika vigezo vya muundo wa lugha na ushawishi. Upungufu kubwa wa vigezo vilivyotolewa na KICD (2021) ni kuwa ni vya jumla mno na havina viashiria bainifu vya utendaji. Hali kadhalika, tafiti kama ya Osore (2022) zina mapungufu ya kimuktadha kwani zilijikita katika shule za upili badala ya shule za msingi.

**Pengo la Utafiti**

Kwa ujumla, mapitio ya tafiti zilizotangulia yanaonyesha kwa uwazi kuwa upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili unahitaji kuzingatia vigezo jumuishi vinavyojumuisha matamshi, sarufi, msamiati, mpangilio wa mawazo, ushirikiano, pamoja na ubunifu wa mwanafunzi. Hata hivyo, jambo kuu ambalo tafiti hizi za awali hazijashughulikia ni ukosefu wa utafiti wa kina unaofafanua, kusanifisha, na kuchanganua vigezo mahsusi vya upimaji vya ndani ya darasa vinavyolingana moja kwa moja na umri, kiwango cha kimaendeleo, na umilisi wa wanafunzi wa Gredi ya Sita nchini Kenya. Miongozo iliyopo ya KICD imebaki kuwa ya jumla, huku tafiti za awali zikijikita katika shule za sekondari au kutoa nadharia za kigeni zisizozingatia mazingira halisi ya darasa la CBC. Utafiti huu unaziba ombwe hili la maarifa kwa kupembua kwa kina vigezo vya upimaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya Sita, na hivyo kupendekeza kuunda zana sahihi, zenye uaminifu, na zinazoweza kutumiwa na walimu kwa urahisi ili kuhakikisha wanafunzi wanahitimisha elimu ya msingi wakiwa na umilisi imara wa Kiswahili fasaha.

**Msingi wa Nadharia**

Nadharia ya Mawasiliano ya Dell Hymes (1974) inasisitiza kuwa mawasiliano si kubadilishana maneno pekee bali ni kitendo cha kijamii kinachojumuisha mazingira yenye maana. Hymes alianzisha dhana ya ethnography of communication competence ili kuelewa jinsi umilisi wa mawasiliano unavyotendeka katika tamaduni na muktadha tofauti (Hymes, 1975). Vipengele vya SPEAKING (Mazingira, Washiriki, Malengo, Mtiririko wa vitendo, Toni, Zana, Kanuni na Aina ya mawasiliano) vinatoa mfumo wa kina wa kutathmini stadi ya kuzungumza kwa kuzingatia muktadha wa kijamii.

Katika elimu, nadharia hii hutumika kubuni mbinu za kufundisha na kupima umilisi wa mawasiliano zinazozingatia mazingira ya kijamii ya wanafunzi (Keating, 2001). Kwa mujibu wa Hymes (2020), stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa Gredi ya sita inaweza kupimwa kupitia midahalo, michezo ya kuigiza, hadithi

na simulizi, kazi za kikundi na ushirikiano na jamii. Njia hizi huwapa wanafunzi nafasi ya kushiriki katika mawasiliano halisi na kujenga ujasiri wa kutumia Kiswahili sanifu.

Nadharia hii inahusiana moja kwa moja na ufunzaji, ujifunzaji na upimaji. Ufunzaji hutokea pale mwalimu anapoweka mazingira ya kijamii ya mawasiliano; ujifunzaji hutokea kupitia mwingiliano wa wanafunzi katika midahalo na kazi za kikundi; na upimaji hutokea mwalimu anapokadiria uwezo wa wanafunzi kushiriki katika mawasiliano yenye maana. Hivyo, nadharia hii inatoa mwongozo wa vitendo wa kuunganisha vipengele hivi vitatu ili kuimarisha stadi ya kuzungumza.

Ingawa imekosolewa kwa kupuuza maarifa ya sarufi, nadharia ya Mawasiliano inafaa kwa utafiti wa upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa Gredi ya sita. Inalingana na mtaala wa umilisi wa KICD unaosisitiza matumizi halisi ya lugha katika muktadha wa kijamii. Kwa hivyo, upimaji haupaswi kuangalia tu sarufi na msamiati bali pia uwezo wa mwanafunzi kutumia Kiswahili sanifu kwa ufanisi katika mazingira ya kijamii (Hymes, 1975; Keating, 2001).

Kwa hivyo, Nadharia ya Umilisi wa Mawasiliano ya Dell Hymes (1967, 1975) ina ufaafu mkubwa katika utafiti huu, kwani inatoa mfumo dhabiti wa kidhana na kiazimio unaomwezesha mtafiti kupembua iwapo vigezo vya upimaji vinavyotumiwa na walimu wa Gredi ya Sita nchini Kenya vinapima matumizi halisi ya lugha kimuktadha badala ya kujikita kwenye usahihi wa kisarufi pekee. Dhana kuu za nadharia hii zinatafsiriwa moja kwa moja katika vigezo mahususi vya upimaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa Gredi ya Sita kupitia mfumo wa *SPEAKING;* ambapo mazingira na kizio cha mawasiliano au mtindo wa mawasiliano zinatafsiriwa kama uwezo wa mwanafunzi kutoa hadithi, michezo ya kuigiza, au midahalo inayolenga mazingira halisi ya darasani au jamii; washiriki na kanuni zinatafsiriwa kama vigezo vya upimaji vinavyoangazia nidhamu ya uzungumzaji, matumizi ya lugha ya heshima na maamkuzi; zana zikipima matumizi ya Kiswahili sanifu, matamshi bora, na msamiati sahihi; ilhali toni na mtiririko zikibainisha ufasaha na mpangilio wa mantiki wa mawazo. Kupitia nadharia hii, mchakato wa upimaji wa mwalimu wa Gredi ya Sita unahama kutoka kupima usahihi wa kiarudhi na kisarufi pekee hadi kupima uwezo kamili wa kijamii na kimawasiliano kulingana na viwango vya utendaji vinavyotarajiwa na mtaala wa umilisi wa KICD.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia muundo wa usorovea fafanuzi ambao unalenga kufafanua sifa za kundi fulani kwa kutumia sampuli iliyoteuliwa kuwakilisha umma lengwa (Kothari, 2004). Muundo huu ulifaa kwa kuwa uliwezesha kuchunguza idadi kubwa ya watafitiwa na kutoa data ya uwakilishi kuhusu upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa Gredi ya Sita. Eneo la utafiti lilikuwa magharibi mwa Kenya (Kakamega, Vihiga, Busia na Bungoma), ambapo upana na mchanganyiko wa jamii ulihakikisha uwakilishi sahihi wa walimu na wanafunzi (Wizara ya Elimu, 2023).

Kundi lengwa lilihusisha walimu wa Kiswahili wa Gredi ya Sita kwa kuwa walimu ndio wapimaji na washiriki wakuu wa mchakato wa upimaji endelezi. Kwa mujibu wa takwimu, kulikuwa na shule 3,207 katika eneo la utafiti, na sampuli ya 355 ilipatikana kwa kutumia fomula ya Taro Yamane (1967) kwa kiwango cha kosa cha 0.05. Usampulishaji tabakishi ulitumiwa kuteua shule za umma na binafsi, kisha usampulishaji nasibu sahili ukatumika kupata majina ya shule, huku walimu wa Kiswahili wakichaguliwa kwa maksudi ili kutoa data mahsusi (Bryman, 2016; Setia, 2016).

Njia kuu za ukusanyaji data zilikuwa uchunguzi darasani, mahojiano na uchanganuzi wa nyaraka. Uchunguzi usioshirikishi ulifanywa ili kupata taswira halisi ya mchakato wa upimaji endelezi wa stadi ya kuzungumza Kiswahili, kwa kuzingatia viwango vinne vya KICD: kuzidisha matarajio, kufikia matarajio, kukaribia matarajio na mbali na matarajio (Cohen et al., 2011; Jwan & Ong'ondo, 2011). Mahojiano ya wazi yalifanywa kwa walimu ili kuongeza kina cha maelezo na kusawazisha data ya hojaji (Fielding & Thomas, 2016).

Vifaa vya utafiti vilijumuisha hojaji, dodoso na mwongozo wa uchanganuzi wa nyaraka. Hojaji zilitumika kukusanya taarifa pana kuhusu maarifa, mielekeo na tajriba za walimu (Johnson & Christensen, 2017). Dodoso lilisaidia kupata majibu ya moja kwa moja kutoka kwa walimu kuhusu ufundishaji na upimaji wa stadi ya kuzungumza (Kumar, 2014). Uchambuzi wa nyaraka ulifanywa kwa mtaala wa Kiswahili wa Gredi

ya Sita na vitendea kazi vya walimu ili kubaini vigezo vya upimaji vya KICD (Jwan & Ong'ondo, 2011; Bowen, 2009).

Uthabiti na utegemezi wa vifaa vya utafiti ulithibitishwa kupitia majaribio ya awali katika shule moja kutoka kila kaunti. Cronbach's alpha ilitumika kupima uthabiti wa vifaa, ambapo kiwango cha 0.6–1 kilionyesha uaminifu (Kothari, 2004). Wahadhiri wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii walitoa ushauri wa kitaalamu ili kuboresha usahihi na ufaafu wa vifaa (Frankfort-Nachmias & Nachmias, 1996; Best & Kahn, 2003).

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia SPSS na NVivo. SPSS ilitumika kuchanganua data ya kiwingiidadi kwa hesabu za marudio, asilimia na chati, huku NVivo ikitumika kuchanganua data ya kithamano kutoka mahojiano na hojaji (Miles et al., 2014; Creswell & Poth, 2018). Mbinu ya kithamano ilihusisha kugawa, kuainisha na kuhusisha vipengele vya data ili kufafanua na kueleza mlingano katika mahusiano (Grbich, 2007; Mathews & Ross, 2010).

Njia ya uchunguzi darasani ilisaidia kupata data pepe kuhusu mazungumzo ya wanafunzi na walimu, ushirikiano wa vikundi na tabia za darasa. Hali hii ilithibitisha majibu ya hojaji na kutoa taswira ya moja kwa moja ya mchakato wa upimaji endelezi wa stadi ya kuzungumza Kiswahili (Cohen et al., 2007). Uchunguzi usioshirikishi ulifaa kwa kuwa uliwezesha mtafiti kumakinikia mchakato bila kuingilia kipindi (Mack et al., 2005).

Mahojiano yaliongeza kina cha maelezo na kutoa utondoti wa vipengele vya upimaji. Maswali wazi yaliruhusu mtafiti kubadilisha au kufafanua maswali kulingana na uelewa wa mtafitiwa, hivyo kuongeza uhalali wa data (Fielding & Thomas, 2016). Mahojiano yalitengewa muda wa dakika 15–20 na majibu yalinakiliwa kwa uchanganuzi wa baadaye.

Kwa jumla, mbinu za utafiti zilizotumika zilihakikisha uthabiti, utegemezi na uhalali wa data kuhusu upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa Gredi ya Sita. Muundo wa usorovea fafanuzi, sampuli ya uwakilishi, njia mseto za ukusanyaji data na uchanganuzi wa kina vilitoa msingi thabiti wa kuelewa vigezo vya upimaji wa stadi ya kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa mtaala wa umilisi (Mertler, 2018). Kwa kurejelea maadili ya utafiti, mtafiti alihakikisha uwazi, haki, na uaminifu kwa kupata vibali vinavyohitajika (kibali cha utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii, National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI), na Mkurugenzi wa Elimu, Kanda ya Magharibi, Kenya), kuheshimu hiari na usiri wa watafitiwa kupitia fomu za ridhaa/idhini ya kushiriki katika utafiti, kulinda usalama wao wa kisaikolojia, na kutambua kazi za wataalamu wengine ipasavyo.

## MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa wanafunzi wa Gredi ya Sita katika muktadha wa Mtaala wa Umilisi. Jumla ya walimu 355 waliteuliwa kupitia usampulishaji maksudi, ambapo 341 (96%) walijaza hojaji kikamilifu. Kiwango hiki cha majibu kilichukuliwa kuwa cha juu na cha kuaminika kwa mujibu wa Kothari (2014), na kilihakikisha uhalali wa matokeo. Mbinu za kukusanya data kwa muda wa miezi miwili na wasaidizi wa mtafiti zilisaidia kufanikisha kiwango hiki cha majibu.

### Taarifa za Kimsingi za Walimu

Walimu wa kike walikuwa asilimia 53.4 na wa kiume asilimia 46.6, ikionyesha usawa wa kijinsia katika sampuli. Aidha, walimu wengi walikuwa na uzoefu wa miaka 7–10 (asilimia 43.1) na miaka 4–6 (asilimia 33.1), jambo lililoongeza uhalali wa data kwa kuwa walimu walikuwa na tajriba ya kutosha (Cohen et al., 2011). Washiriki wote walifundisha Kiswahili katika Gredi ya Sita, na asilimia 78.3 walifundisha pia gredi za chini, hali iliyowapa mtazamo mpana wa mfululizo wa stadi za lugha. Tajriba hii ilihakikisha kuwa data iliyokusanywa inatokana na uzoefu wa kina wa kitaalamu, na hivyo kuongeza uaminifu wa matokeo.

### Vigezo vya Upimaji wa Stadi ya Kuzungumza Kiswahili vya KICD katika Gredi ya Sita

Kwa kurejelea KICD (2021), upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya Sita chini ya Mtaala wa Umilisi (CBC) unazingatia vigezo sita vikuu: ufasaha na matamshi, sarufi na msamiati, mpangilio wa mawazo, ushirikiano katika mazungumzo, ubunifu na ushawishi, pamoja na matumizi ya ishara za mwili. Vigezo hivi vina misingi thabiti ya kitaaluma, ambapo Hymes (1972) anasisitiza umilisi wa kijamii na kilugha katika ushirikiano na matumizi ya lugha kimuktadha, huku Mwangi (2021) akibainisha kuwa matamshi sahihi

na lafudhi inayofaa hujenga ujasiri wa mwanafunzi. Aidha, Njogu et al. (2006) na Koros na Achieng (2023) wanaeleza kuwa sarufi na msamiati tajiri wa Kiswahili sanifu ndio msingi wa mawasiliano ya kitaaluma, huku Halliday (1994) akisisitiza kuwa lugha hutimiza kazi ya kiidadi kupitia mpangilio wa mawazo wenye mantiki na unaozingatia uhalisia wa kijamii na kiutamaduni. Mwishowe, Njogu et al. (2006), Halliday (1994), na Ochieng (2024) wanakubaliana kuwa ubunifu, ushawishi, na matumizi ya methali na taswira ni kiini cha kukuza stadi za Karne ya 21 zinazotawala mtaala wa KICD.

**Walimu Kuhudhuria Warsha Kuhusu Mtaala wa Umilisi**

Katika utafiti huu, walimu wa Gredi ya Sita waliulizwa ikiwa wamewahi kuhudhuria warsha ya Kiswahili ya Mtaala wa Umilisi na ikiwa mtaala una mwongozo wa upimaji wa stadi ya kuzungumza. Uchanganuzi wa data ya kimaelezo unaonyesha kuwa matamshi bora na sauti vilipata asilimia 25.6, kiwango kilicholingana sawia na mijadala na mawasiliano ya makundi yaliyopata asilimia 25.6. Vitate na vitanzandimi vilipata asilimia 10.3, huku suala la jinsi ya kujibu maswali au kauli likifuatia kwa asilimia 7.7. Maeneo ya maigizo na michezo ya kuigiza, kukariri mashairi, nyimbo, fasihi (methali na tamathali za usemi), sarufi na msamiati, pamoja na tathmini na upimaji yote yalipata asilimia 5.1 kila kimoja. Hatimaye, masuala ya ujasiri wa kuzungumza pamoja na nyenzo na mbinu za ufundishaji yalipata asilimia ya chini zaidi ya 2.6 kila kimoja.

Matokeo haya yanadhihirisha kuwa maeneo yenye nguvu ni ufasaha na matamshi pamoja na mpangilio wa mawazo, yaliyopata asilimia kubwa zaidi, yakionyesha kuwa walimu walisisitiza sana usahihi wa matamshi na mijadala ya makundi. Hii inathibitisha maoni ya Hymes (1972) na Mwangi (2021) waliosisitiza kuwa lafudhi sahihi huongeza ujasiri wa mwanafunzi, pamoja na mtazamo wa Halliday (1994) kuhusu mpangilio wa mawazo katika CBC. Hata hivyo, kuna mapengo yanayohitaji kuimarishwa, kwani sarufi na msamiati vilipata asilimia 5.1 pekee ingawa wataalamu kama Njogu et al. (2006) na Koros na Achieng (2023) walisisitiza kuwa ni msingi wa mawasiliano ya kitaaluma. Vivyo hivyo, ushirikiano na hadhi pamoja na vipengele vya ubunifu kupitia fasihi na maigizo vilipata asilimia ndogo. Kwa hivyo, mapendekezo ya kitaaluma yanahimiza kuendeleza mafunzo ya kina kuhusu sarufi, msamiati, na ujasiri wa wanafunzi ili kuambatana na vigezo vya KICD.

**Mwongozo Kuhusu Upimaji wa Stadi ya Kuzungumza katika Mtaala wa KICD**

Kwanza, kuhusu ufahamu wa walimu juu ya uwepo wa mwongozo wa KICD, data inaonyesha kuwa walimu 291 (85.3%) walithibitisha uwepo wake (“Ndiyo”), wakati walimu 50 (14.7%) walisema kuwa mwongozo huo haupo (“La”). Takwimu hizi zinaonyesha uelewa chanya kwa walimu wengi, jambo linaloashiria kuwa KICD imefanikiwa kutoa misingi na mwelekeo wa upimaji. Hata hivyo, asilimia 14.7 inayokanusha inaashiria kuwa bado kuna haja ya kuongeza uelewa na ufikiaji wa nyaraka za mtaala au mafunzo ili kuhakikisha walimu wote wanautumia kwa ufanisi. Matokeo ya utafiti yanayobainisha kuwa asilimia 14.7 ya walimu hawana uelewa au ufikiaji wa mwongozo wa upimaji wa KICD yanaoana moja kwa moja na tahadhari za Bachman (1990) na Weir (2005) kuhusu vikwazo vya utekelezaji wa tathmini, kwani ingawa mwongozo huo unakubaliwa na wataalamu mbalimbali (Hymes, 1972; Halliday, 1994; Njogu et al., 2006; Mwangi, 2021; Koros & Achieng, 2023; Ochieng, 2024) kwa kuwainisha wanafunzi katika ngazi nne za utendaji kupitia vigezo vya kimilisi na kimazingira vya BECF, udhaifu wake mkuu unajidhihirisha darasani ambapo ukosefu wa mafunzo na maandalizi ya walimu unahatarisha ufanisi na uaminifu wa upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya Sita.

Pili, walimu waliorodhesha vipengele vya KICD vinavyoongoza upimaji huo ambapo matamshi na ufasaha wa lugha vilipata asilimia 24.5, vikifuatiwa na mbinu za upimaji kama mitihani, kazi mradi na mijarabu kwa asilimia 20.4. Fasihi simulizi na utamaduni (methali, nahau, adabu) zilipata asilimia 18.4, mwingiliano kupitia mijadala na maigizo ukapata asilimia 16.3, miundo ya lugha kama sarufi na msamiati ikapata asilimia 12.2, na viwango vya matarajio au *rubrics* vikapata asilimia ndogo zaidi ya 8.2. Data hii inaonyesha kuwa upimaji unavuka mipaka ya mitihani ya kijadi na unasisitiza muktadha wa kijamii na utambulisho wa kitamaduni. Matokeo haya yanaafikiana na Osore (2022) aliyebaini ufanisi wa nyenzo za kusikiliza na kuona, pamoja na Melly et al. (2023) walioonyesha kuwa majadiliano ya makundi hufanikisha upimaji huo. Hata hivyo, udhaifu upo

katika utekelezaji wa miundo ya lugha na rubrik thabiti ambazo zilitajwa kwa kiwango cha chini, ikilinganishwa na umuhimu ulioelezwa na Njogu et al. (2006), Koros na Achieng (2023), na Weir (2005).

Kwa hivyo, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti yanayobainisha kuwa walimu wanazingatia matamshi, mbinu za upimaji, fasihi simulizi, na mwingiliano (Osore, 2022; Melly et al., 2023) yanaoana na mfumo wa KICD na BECF pamoja na nadharia za wataalamu (Hymes, 1972; Halliday, 1994; Njogu et al., 2006; Mwangi, 2021; Koros & Achieng, 2023; Ochieng, 2024) katika kupima stadi ya kuzungumza kimuktadha, lakini kiwango duni cha matumizi ya miundo ya lugha na rubrik (8.2%) kinathibitisha tahadhari za Bachman (1990) na Weir (2005) kuhusu uwepo wa udhaifu mkubwa wa kiutekelezaji na ukosefu wa zana thabiti za utuzaji alama darasani.

Tatu, mbinu zilizopendekezwa na walimu ili kuboresha uwezo wa wanafunzi katika kuzungumza Kiswahili ziliongozwa na mbinu shirikishi (mijadala, makundi, mahojiano) kwa asilimia 34.6, zikifuatiwa na sanaa na fasihi simulizi (nyimbo, mashairi, hadithi) kwa asilimia 23.1. Usomaji na uandishi saidizi (vitabu, magazeti, insha) ulipata asilimia 15.4, uwasilishaji wa hadhara (gwarideni, hotuba, habari) ukapata asilimia 11.5, huku sera za shule kama Siku ya Kiswahili pamoja na teknolojia na rekodi za sauti zikitajwa kwa asilimia 7.7 kila kimoja. Mbinu shirikishi na sanaa/fasihi ndizo zinazopewa kipaumbele kikubwa, zikionyesha kuwa wanafunzi wanajifunza vizuri kupitia mwingiliano na utamaduni kulingana na wataalamu kama Njogu et al. (2006), Ochieng (2024), na Hymes (1972). Maeneo yanayohitaji kuimarishwa ni usomaji/uandishi saidizi, uwasilishaji hadhara, sera za shule, na teknolojia ambazo hazijapewa uzito mkubwa bado.

Nne, katika kukuza mazungumzo ya Kiswahili darasani, walimu walibainisha kuwa wanatumia mijadala na mazungumzo ya vikundi kwa asilimia 31.8, fasihi simulizi (vitendawili, hadithi, mashairi) kwa asilimia 20.5, na matamshi, sauti tata au kusoma kwa sauti kwa asilimia 18.2. Uwasilishaji na hotuba mbele ya darasa zilipata asilimia 11.4, huku maigizo/majukumu pamoja na teknolojia kupitia projekta zikipata asilimia 9.1 kila kimoja. Mijadala na vikundi ndiyo njia kuu, ikionyesha mabadiliko kuelekea ufundishaji unaomlenga mwanafunzi (learner-centered). Walimu hutumia michezo ya lugha kama vitendawili kukuza kufikiri na kutoa sentensi za kuzungumza ili kupunguza uoga, jambo linaloafikiana na nadharia ya Halliday (1994). Matokeo ya utafiti yanayobainisha kuwa walimu wanatumia zaidi mbinu shirikishi kama mijadala ya vikundi, fasihi simulizi, na matamshi ili kukuza ufundishaji unaomlenga mwanafunzi yanaoana kikamilifu na misingi ya KICD na BECF pamoja na nadharia za Hymes (1972), Halliday (1994), Njogu et al. (2006), Mwangi (2021), Koros na Achieng (2023), na Ochieng (2024) zinazosisitiza upimaji wa kimilisi na kimazingira, ingawa mafanikio ya mbinu hizi darasani bado yanatishiwa na udhaifu wa kiutekelezaji katika matumizi ya zana thabiti za rubrik kama walivyotahadharisha Bachman (1990) na Weir (2005).

Mbinu zilizogunduliwa kuwa na matokeo mazuri katika kuwafundisha wanafunzi kuzungumza Kiswahili fasaha ziliongozwa na mijadala na majadiliano ya vikundi kwa asilimia 27.9, zikifuatiwa na uigizaji na uwasilishaji kwa asilimia 23.3. Sarufi na fani za lugha (silabi, matamshi, ngeli, viwakilishi) zilipata asilimia 16.3, teknolojia na vyombo vya habari (projekta, video, magazeti) vikapata asilimia 14.0, mbinu za kichocheo (chemshabongo, ziara za nyanjani) zikitajwa kwa asilimia 11.6, na sanaa (nyimbo na hadithi) kwa asilimia 7.0. Uchanganuzi huu unaonyesha mwelekeo wa "Uigaji wa Kitaalamu" kama kuiga wanahabari, mbinu ya kisasa inayomandaa mwanafunzi katika nyanja za kikazi na uelewa mpana wa mfumo wa lugha kulingana na Ochieng (2024) na Koros na Achieng (2023).

Kwa hivyo, matokeo ya utafiti yanayobainisha kuwa mbinu shirikishi kama mijadala, uigizaji, uigaji wa wanahabari, na matumizi ya teknolojia ndizo zenye matokeo mazuri zaidi katika kuwafundisha wanafunzi kuzungumza Kiswahili fasaha yanayoshabihiana kikamilifu na misingi ya KICD na BECF pamoja na nadharia za Hymes (1972), Halliday (1994), Koros na Achieng (2023), na Ochieng (2024) zinazosisitiza ufundishaji unaomlenga mwanafunzi na upimaji wa kimilisi katika mazingira halisi ya kijamii, huku pia ikishughulikia changamoto za kiutekelezaji zilizotahadharishwa na Bachman (1990) na Weir (2005) kwa kuimarisha utendaji na uelewa mpana wa mfumo wa lugha darasani.

Mwisho, tukirejelea suala la walimu kuhudhuria warsha za Kiswahili za Mtaala wa Umilisi, matokeo

yanaonyesha kuwa walimu 259 (76.0%) wamehudhuria na kupata mafunzo, jambo linaloashiria kuwa utekelezaji wa mtaala wa KICD unapata msingi thabiti nchini. Hata hivyo, kuna udhaifu unaojitokeza kwani walimu 82 (24.0%) hawakuwahi kuhudhuria warsha hizi, hali inayoweza kuathiri usawa na ubora wa utekelezaji kwa sababu ya changamoto za rasilimali, umri, umbali, au gharama. Mikakati ya makusudi inahitajika ili kuhakikisha walimu wote wanapata mafunzo haya ili kuondoa pengo la ujuzi na kuimarisha usawa wa elimu.

Kwa hivyo, matokeo ya utafiti yanayobainisha kuwa asilimia 76.0 ya walimu wamehudhuria warsha za Mtaala wa Umilisi yanaoana na mwelekeo wa KICD na BECF pamoja na maoni ya wataalamu kama Hymes (1972), Halliday (1994), Njogu et al. (2006), Mwangi (2021), Koros na Achieng (2023), na Ochieng (2024) katika kuweka msingi thabiti wa kukuza umilisi wa mwanafunzi wa Gredi ya Sita katika stadi ya kuzungumza Kiswahili. Hata hivyo, kundi la asilimia 24.0 ya walimu ambao hawajawahi kupata mafunzo hayo linathibitisha kikamilifu tahadhari za Bachman (1990) na Weir (2005) kuhusu udhaifu wa kiutekelezaji na athari za ukosefu wa mafunzo ya kina kwa walimu. Ombwe hili la mafunzo linahatarisha uwezo wa walimu kutumia zana na rubrik thabiti za upimaji, jambo linaloweza kuleta athari katika usawa, uaminifu, na ubora wa tathmini endelezi za darasani kote nchini.

**Muhtasari wa Utafiti**

Matokeo ya vigezo vya upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya Sita yanaonyesha kuwa mwongozo wa KICD (2021, uk.42) umejikita katika vipengele sita vikuu: ufasaha na matamshi, sarufi na msamiati, mpangilio wa mawazo, ushirikiano na hadhi, ubunifu na ushawishi, pamoja na matumizi ya ishara za mwili. Kwa mujibu wa KICD, "mwanafunzi anatathminiwa kwa kuzungumza kwa ufasaha, kutumia sarufi na msamiati sahihi, kupanga mawazo kwa mantiki, kushirikiana na hadhira kwa heshima, na kuonyesha ubunifu na ushawishi katika mawasiliano" (KICD, 2021, uk.42). Hii inathibitisha kuwa vigezo vya tathmini vinahusiana moja kwa moja na falsafa ya CBC ya kupima kile mwanafunzi anajua na anaweza kufanya.

Zaidi ya hayo, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa walimu wengi (85.3%) wanakubali kuwa mtaala wa KICD una mwongozo wa upimaji wa stadi ya kuzungumza, ingawa 14.7% hawana ufahamu wa mwongozo huo. Hali hii inathibitisha hoja ya Bachman (1990) kwamba upimaji wa lugha unapaswa kutumia mbinu mseto ili kuonyesha uwezo halisi wa mwanafunzi, na maoni ya Weir (2005) kwamba rubrik thabiti na nyenzo za kisasa ni msingi wa uthabiti wa tathmini. Kwa hivyo, ingawa mwongozo wa KICD una ubora wa kuunganisha nadharia za kitaaluma na kijamii (Hymes, 1972; Halliday, 1994; Njogu et al., 2006; Mwangi, 2021; Koros & Achieng, 2023; Ochieng, 2024), bado kuna udhaifu katika ufikishaji na utekelezaji wake thabiti kwa walimu wote.

Matokeo ya warsha kwa walimu wa Kiswahili yanaonyesha kuwa maeneo yaliyosisitizwa zaidi ni matamshi bora na sauti (25.6%) pamoja na mijadala na mawasiliano ya makundi (25.6%). Hii inalingana na maoni ya Hymes (1972) kuhusu ufasaha wa mawasiliano na Halliday (1994) aliyesisitiza kazi ya ideational ya lugha. Hata hivyo, vipengele vya sarufi na msamiati (5.1%) na ujasiri wa kuzungumza (2.6%) vilipata nafasi ndogo, jambo linaloonyesha pengo kati ya mafunzo ya warsha na umuhimu wa kitaaluma. Njogu et al. (2006) na Koros na Achieng (2023) walisisitiza kuwa Kiswahili sanifu na msamiati tajiri ni msingi wa mawasiliano ya kitaaluma, huku Mwangi (2021) akiongeza kuwa lafudhi sahihi huongeza ujasiri wa mwanafunzi katika mawasiliano ya umma.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili katika Gredi ya Sita unasisitiza zaidi matamshi na mijadala ya makundi, lakini unakosa uzito katika sarufi, msamiati na rubriki thabiti. Walimu wanapendekeza mbinu shirikishi na fasihi simulizi kama njia bora za kuboresha uzungumzaji. Hivyo, kuna haja ya kuimarisha mafunzo ya walimu, kusambaza mwongozo wa KICD kwa usawa, na kuendeleza mbinu shirikishi ili kuhakikisha kuwa upimaji wa stadi ya kuzungumza unakuwa thabiti, shirikishi na unalingana na mahitaji ya mtaala wa umilisi.

Aidha, utafiti ulibainisha na kufafanua viashiria mahsusi vya utendaji kama vile matamshi na ufasaha, mpangilio wa mawazo, ushirikiano na maadili, mbinu shirikishi, pamoja na matumizi ya rubriki ambavyo vinaziba pengo kati ya vigezo vya jumla vya KICD na utekelezaji

halisi wa upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili darasani.

**Mapendekezo:** Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, taasisi za elimu ziharakishe usambazaji wa nyaraka za mtaala, zipanue maudhui ya warsha za walimu ili yajumuishe sarufi na msamiati, na ziingize matumizi ya teknolojia ili kuimarisha upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili.

Aidha, utafiti unapendekeza kuwa Wizara ya Elimu na KICD ziongeze ufikiaji wa mwongozo wa upimaji na kuimarisha warsha za mara kwa mara kwa ushirikiano na Tume ya Kuajiri Walimu, vyuo vikuu, na taasisi za mafunzo ya walimu ili kuwajengea walimu wote uwezo thabiti wa kutumia rubriki na kutekeleza vigezo vyote vya upimaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa usawa darasani.

Mwisho, tafiti za baadaye zinaweza kuchunguza jinsi zana za kidijitali zinavyoweza kutumika kufundishia na kupimia stadi ya kuzungumza Kiswahili katika shule za vijijini zenye uhaba wa rasilimali.

**MAREJELEO**


Ahmad, M., Qasim, H. M., & Khushi, Q. (2019). Specifying criteria for the assessment of speaking skill: A library-based review. *International Journal of Educational Sciences, 24*(1–3), 23–33. https://doi.org/10.31901/24566322.2019/24.1-3.1075

Bachman, L. F. (1990). *Fundamental considerations in language testing*. Oxford University Press.

Best, J. W., & Kahn, J. V. (2003). *Research in education* (9th ed.). Allyn & Bacon.

Bimpong, W. K. (2020). Supporting the speaking development of students in a Swahili-as-a-foreign-language (SFL) classroom. *Ghana Journal of Linguistics,* 9(1), 1–17. https://doi.org/10.4314/gjl.v9i1.1

Bowen, G. A. (2009). Document analysis as a qualitative research method. *Qualitative Research Journal,* 9(2), 27–40. https://doi.org/10.3316/QRJ0902027

Bryman, A. (2016). *Social research methods* (5th ed.). Oxford University Press.

Care, E., Griffin, P., & Wilson, M. (Eds.). (2018). *Assessment and teaching of 21st century skills: Research and applications*. Springer. https://doi.org/10.1007/978-3-319-65368-6

Cohen, L., Manion, L., & Morrison, K. (2007). Observation. In *Research methods in education* (6th ed., pp. 396–412). Routledge. https://doi.org/10.4324/9780203029053-29

Cohen, L., Manion, L., & Morrison, K. (2011). *Research methods in education* (7th ed.). Routledge.

Creswell, J. W., & Poth, C. N. (2018). *Qualitative inquiry and research design: Choosing among five approaches* (4th ed.). SAGE.

Đorđević, J. (2025). Rubrics in the assessment of EAP speaking skills supported by mobile assisted language learning. *ESP Today, 13*(1), 91–112. https://doi.org/10.18485/esptoday.2025.13.1.5

Eliyasun, E., Rosnija, E., & Salam, U. (2018). Improving student's speaking ability through guided questions. *Jurnal Pendidikan dan Pembelajaran Khatulistiwa,* 7(1). https://jurnal.untan.ac.id/index.php/jpdpb/article/view/23769

Fielding, N., & Thomas, H. (2016). Qualitative interviewing. In N. Gilbert & P. Stoneman (Eds.), *Researching social life* (4th ed., pp. 281–300). SAGE Publications.

Frankfort-Nachmias, C., & Nachmias, D. (1996). *Research methods in the social sciences* (5th ed.). Arnold.

Grbich, C. (2007). *Qualitative data analysis: An introduction*. SAGE.

Halliday, M. A. K. (1994). *An introduction to functional grammar* (2nd ed.). Edward Arnold.

Hymes, D. H. (1972). On communicative competence. In J. B. Pride & J. Holmes (Eds.), *Sociolinguistics: Selected readings* (pp. 269–293). Penguin.

Hymes, D. H. (1974). *Foundations in sociolinguistics: An ethnographic approach*. University of Pennsylvania Press.

Humphry, S., Heldsinger, S., & Dawkins, S. (2017). A two-stage assessment method for assessing oral language in early childhood. *Australian Journal of Education, 61*(2), 124–140. https://doi.org/10.1177/0004944117712777

Johnson, B., & Christensen, L. (2017). *Educational research: Quantitative, qualitative, and mixed approaches* (6th ed.). SAGE.

Jwan, J. O., & Ong'ondo, C. O. (2011). *Qualitative research: An introduction to principles and techniques*. Moi University Press.

Kenya Institution of Curriculum Development. (2017). *Basic education curriculum framework*. Kenya Institute of Curriculum Development.

Kenya Institution of Curriculum Development. (2021). *Upper primary level designs*. Kenya Institute of Curriculum Development.

Koros, D. P., & Achieng, S. D. S. B. (2023). Competency based curriculum preparedness: Perception of teachers in selected public and private primary schools in Kenya. *IJRDO – Journal of Educational Research, 9*(6), 6–14. https://doi.org/10.53555/er.v9i6.5755

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd ed.). New Age International.

Krashen, S. D. (1982). *Principles and practice in second language acquisition*. Pergamon.

Kumar, R. (2014). *Research methodology: A step-by-step guide for beginners* (4th ed.). SAGE.

Lightbown, P. M., & Spada, N. (2013). *How languages are learned* (4th ed.). Oxford University Press.

Lukindo, J. J. (2016). Exploring competence-based education (CBE) in rural secondary schools in Tanzania: English language teachers' conceptions and experiences. *Journal of Education and Practice, 7*(29), 62–67. https://files.eric.ed.gov/fulltext/EJ1118886.pdf

Luoma, S. (2004). *Assessing speaking*. Cambridge University Press.

Mack, N., Woodsong, C., MacQueen, K. M., Guest, G., & Namey, E. (2005). *Qualitative research methods: A data collector's field guide*. Family Health International.

Mathews, B., & Ross, L. (2010). *Research methods: A practical guide for the social sciences*. Pearson.

Melly, R., Okari, F., & Oseko, A. (2023). Testing speaking skills through writing and learners' speaking competence in selected secondary schools in Wareng' Sub-County, Uasin Gishu County, Kenya. *African Journal of Education, Science and Technology, 7*(3), 421–427. https://www.ajol.info/index.php/ajedscitech/article/download/254558/240538/606295

Mertler, C. A. (2018). *Introduction to educational research* (2nd ed.). SAGE.

Miles, M. B., Huberman, A. M., & Saldaña, J. (2014). *Qualitative data analysis: A methods sourcebook* (3rd ed.). SAGE.

Mwangi, P. (2021). *Pronunciation and confidence in Kiswahili communication* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository.

Njogu, K., Momanyi, C., & Mathooko, M. (Eds.). (2006). *Fasihi simulizi ya Kiswahili*. Twaweza Communications.

Nyamai, M. (2023). *Assessment of Kiswahili communication skills under the competency-based curriculum in primary schools in Machakos County, Kenya* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.

Ochieng, S. (2024). *Creativity and persuasion in oral Kiswahili communication among primary school learners* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.

Opondo, R. O., Afwande, J., & Kamau, L. N. (2023). Challenges facing implementation of competency-based assessment in Kenyan primary schools: Case of Kajiado County. *International Journal of Education and Research, 11*(1), 21–32. https://www.ijern.com/journal/2023/January-2023/03.pdf

Osore, J. L. (2022). *Matumizi ya nyenzo za kusikiliza na kuona katika ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi katika shule za upili, Kaunti ya Kiambu, Kenya* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/bitstreams/a668553d-eaed-43a2-be00-bde7f6c200d8/download

Otieno, M., & Machani, A. (2022). Teachers' competencies in assessment of competency-based curriculum among Grades 1, 2, and 3 in Langata Sub-County, Kenya. *International Journal of Humanities, Social Sciences and Education, 9*(12), 37–45. https://doi.org/10.20431/2349-0381.0912005

Özdil, Ş., & Duran, E. (2023). Development of persuasive speaking skills rubrics for primary school fourth grade students. *International Journal of Education and Literacy Studies, 11*(1), 59–67. https://doi.org/10.7575/aiac.ijels.v.11n.1p.59

Setia, M. S. (2016). Methodology series module 5: Sampling strategies. *Indian Journal of Dermatology, 61*(5), 505–509. https://pmc.ncbi.nlm.nih.gov/articles/PMC5029234/

Skolverket. (2019). *Curriculum for the preschool: Lpfö 18*. Swedish National Agency for Education. https://www.skolverket.se/download/18.6bfaca41169863e6a65d897/1553968298535/pdf4049.pdf

Weir, C. J. (2005). *Language testing and validation: An evidence-based approach*. Palgrave Macmillan. https://doi.org/10.1057/9780230514577

Zuhriyah, M. (2017). Storytelling to improve students' speaking skill. *English Education: Jurnal Tadris Bahasa Inggris, 10*(1), 119–134. https://doi.org/10.24042/ee-jtbi.v10i1.879